



Ngamia wazima waliolishwa chumvi; wenye afya njema



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Watayarishi:

Kuria S. G., Aila Y. K., Tura I. na H. K. Walaga

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Marsabit

S.L.P. 147-60500

Simu: 069-2040/2220

Nukulishi: 069-2220

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 45 /2008

Shilingi 20 za Kenya

**Jinsi ya kutengeneza na
kulisha 'chumvi kuria'
kwa ngamia**



Utangulizi

Ukosefu wa madini ni mojawapo wa sababau zinazozorotesha mazao ya mifugo. Chemchemi za chumvi za kiasili ni nadra na hazifikiki. Uhaba wa madini huzuia ulaji mzuri na matatizo ya chakula kusagwa mwilini na kupelekea ukuaji mbaya na uhaba wa maziwa.

'Chumvi kuria' inayotengenezewa nyumbani imetambulika kuongeza maziwa na kukua haraka kwa ndama kwa asilimia 30 na pia huimarisha hali ya afya ya mnyama.

Jinsi ya kutayarisha 'Chumvi Kuria'

Hatua ya kwanza

Okota mifupa ya zamani au mibichi. Kama ni mibibichi ikaushe kwa juma moja kuondoa kaboni.

Hatua ya pili

Ichome mifupa hiyo katika chombo wazi kwa masaa mawili ili kuifanya iwe laini na kua viumbe hai.



Hatua za kuchoma

Hatua ya tatu

Saga mifupa kwa kutumia jiwe au visagio vingine

Hatua ya nne

Chukua mchanga kutoka jangwa ya Chalbi na uondoe mawe.

NB: Chumvi chembe chembe za Red Magadi au ya nyumbani itumike iwapo hamna mchanga wa Chalbi japo hii huathiri kiwango cha ubora wa 'Chumvi Kuria'.

Hatua ya tano

Pima kilo 2 za mseto wa mifupa na uchanganye na kilo 3 za chumvi ya jangwa la Chalbi ili kukupa 'Chumvi Kuria' (vitengo mbili vya mifupa kwa 3 vya chumvi ya jangwa la Chalbi)

Kuwalisha ngamia 'chumvi kuria'

Mwaga 'Chumvi Kuria' katika hori ya kulishia (ya mti au nusu pipa) na uwaruhusu ngamia kuramba peke yao au changanya na maji ya kunywa. Hakikisha kuwa kuna chumvi kuria kwenye hori kila wakati.



Ngamia wakiramba chumvi kuria


Faida za kuwalisha 'Chumvi Kuria'



Kushoto: maziwa kidogo bila povu iwapo hamna chumvi
Kulia: maziwa mengi, povu jingi iwapo kuna chimvi Kuria

Faida zingine

- Hali ya afya ya mnyama huimarika
- Zaidi ya asilimia 30 ya kukua kwa ndama
- Jike hupata mimba haraka
- Ngamia huhitaji maji mara chache.



Ndama wakubwa wenye afya nzuri